# DARASA LA SITA - MWAKA 2016
# KISWAHILI

**_Muda: Saa 1 Dakika 46_**

**_Chagua jibu mwafaka kujazia pengo._**

Nilikuwa na umri wa __1__ ishirini na __2__. Maisha __3__ bado __4__ na matumaini yangu yalikuwa __5__ sana. Katika afya nilikuwa nimejaa utomvu wa uzima na katika moyo furaha. Kichwa __6__ bado kuota __7__ na ugonjwa __8__ mbali na mwili. Uchovu ulikuwa kitu __9__ kukiona mwilini. Nilikuwa katika mwanzo tu __10__ maisha: bado sijafika katikati __11__ mwisho wake. Kurasa __12__ maisha yangu yaliyopita zilikuwa __13__ na matendo haba yaliyoandikwa juu yake katika wakati __14__ nyuma yalikuwa hayawezi kuwatamanisha wengine kuyanakili wala kuniridhisha mimi __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mwaka | B. miaka | C. myaka | D. miyaka |
| 2. | A. misaba | B. misita | C. mitisa | D. saba |
| 3. | A. yalikuwa | B. ilikuwa | C. zilikuwa | D. ulikuwa |
| 4. | A. mpya | B. vipya | C. mipya | D: mapya |
| 5. | A. mengi | B. mingi | C. nyingi | D. vingi |
| 6. | A. kilikua | B. kilikuwa | C. ilikuwa | D. ulikuwa |
| 7. | A. umbu | B. mbu | C. mvi | D. nvi |
| 8. | A. yalikuwa | B. ulikua | C. kilikuwa | D. ulikuwa |
| 9. | A. ngeni | B. geni | C. kigeni | D. mgeni |
| 10. | A. wa | B. ya | C. la | D. cha |
| 11. | A. wala | B. ila | C. ili | D. bila |
| 12. | A. ya | B. za | C. wa | D. la |
| 13. | A. mingi | B. vichache | C. mengi | D. chache |
| 14. | A. ya | B. wa | C. za | D. cha |
| 15. | A. mwenye | B. wenyewe | C. yenyewe | D. mwenyewe |



Test compiled by Schools Net Kenya, Term 1, 2016 | Available online at www.schoolsnetkenya.com
Contact details: E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 0711882227

***Kwa swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Salamu ya heshima kwa mtu anayekuzidi umri ni ______

A. Masalkheri

B. Alamsiki

C. Shikamoo

D. Asalaam Aleikum

17. Andika ngeli ya jina kalamu.

A. A-WA
B. I-ZI
C. KI-VI
D. M-WA

18. Anayewakilisha nchi yetu huko Uchina kwa niaba ya Rais ni:-

A. Ustadh
B. Bibi
C. Yahe
D. Balozi

19. Andika tarakimu 100,000 kwa maneno.

A. Laki moja

B. Milioni moja

C. Mia moja

D. Elfu

20. Chagua kiashiria radidi kwa usahihi.

Wachezaji walitoka kula kule ______

A. kijiji

B. vijiji

C. vijijini

D. mji

21. ***Kamilisha sentensi kwa istiara mwafaka.***

Barabara hii ni ______ angalia kuruba zote hizo.

A. ndefu
B. nyoka
C. refu
D. lami

***Tumia vivumishi vya pekee kwa usanifu kujaza uwazi.***

22. Kinyozi hunyoa nywele ______

A. zozote
B. zote
C. yoyote
D. wowote

***Tumia tanakali za sauti kwa usahihi.***

23. Kuku alichinjwa ______

A. fyu
B. mwa
C. rwa
D. chwa

24. Kiungo aina ya madini kinachotumika kuongeza ladha katika chakula ni ______

A. tangawizi

B. iliki

C. chumvi

D. karafuu

***Kamilisha methali kwa usahihi***

25. Ibilisi wa mtu ni ______

A. mtu

B. shetani

C. rafiki

D. utumwa

***Tumia kivumishi "ngi" kwa njia sahihi.***

26. Mama alinipa uji ______ ninywe.

A. mingi

B. mwingi

C. nyingi

D. zingi

27. ______ ni kikembe wa punda.

A. Kiongwe

B. Kipara

C. Kipunda

D. Kibui

28. Tumia tasfida badala ya maneno uliyopewa

Mwanauzi amezaa ______

A. alienda msalani

B. amepiga maji

C. amejifungua

D. ameaga dunia

29. ***Tumia kiambishi sahihi cha amba.***

Samaki amba ______ walivuliwa wameuzwa.

A. yo

B. ye

C. zo

D. o

30. Meli hii inaendeshwa na ______ mahiri.

A. dereva

B. nahodha

C. rubani

D. utingo

*Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali 31-40.*

1. Kitenge nisiye shaka, natokea kiwanjani.
Tumbo langu linawaka, kwa fikira za moyoni.
Kila pembe nimesaka, nyikani na maporini.

2. Ndege ninamtafuta, wa kutulia tunduni.
Moyo unanipapata, kwa kutembea porini.
Ndege asiyemata, sijamwona asilani.

3. Nimefika Githurai, nikaingia porini.
Nikatega barawai, nikamnasa mtini.
Kumbe ndege hafai, kahamia Kasarani.

4. Nikaenda Rusinga, visiwa vyetu ziwani.
Nikashika njiwamanga, nikafurahi moyoni.
Siku mbili akaringa, kenda zake mafichoni.

5. Nikenda tega Masaku, kwenye hewa milimani.
Nikampata kasuku, mwenye sauti laini.
Maneno kama chiriku, na uwongo mitaani

31. Jina lifaalo la shairi hili ni:-
A. Tarbia
B. Tashtita
C. Tathlitha
D. Malenga

32. Shairi hili lina mishororo mingapi?
A. 16
B. 15
C. 8
D. 64

33. Mtunzi wa shairi hili ajiita:-
A. Kasuku
B. Njiwamanga
C. Barawai
D. Kitenge

34. Katika ubeti wa tatu mishororo wa kibwagizo kuna mizabi ngapi?
A. 16
B. 15
C. 64
D. 32

35. Katika ubeti uliofunga shairi hili vina vya kati na vya mwisho ni:-
A. ka, ni
B. ku, ni
C. ta, ni
D. ai, ni

36. Mtunzi aliwanasa ndege wangapi?
A. 2
B. 1
C. 3
D. 5

37. Ni yupi kati ya ndege wote alitulia?
A. Njiwamanga
B. Kasuku
C. Barawai
D. Hakuna

38. Ubeti wa pili una mizani ngapi?
A. 16
B. 24
C. 32
D. 48

39. Kulingana na shairi, mtunzi alimtaka ndege wa:-
A. kutulia tunduni
B. kutembea porini
C. sijamwona asilani
D. uwongo mitaani

40. Ni kina kipi hakikutumika katika shairi hili?
A. nga
B. ta
C. pa
D. ai

***Soma ufahamu kisha ujibu maswali 41-50.***

"Bila ya mtu kuichukua ningalikuwa nayo!" Wingo akafikiri. Akawasha kiko chake na kuanza kukivuta hali anaangalia juu akifikiri. Bila shaka, Akaanza kufikiri moyoni. Rafaili au Maria wote wanaweza kuwa wameiandaa sigara ile ya sumu. Walitaka mzee yule afe ili waweze kuoana. Na sigara yenyewe iliyopotea labda Maria aliichukua. Je, ni nani huyu alinipigia simu kunijulisha mzee Yakobo amefariki? Mle ndani mlikuwa na wanawake tu, nao hakuna hata aliyetoka nje. Je, inawezekana wakawa wamefanya siri ili wamwue mzee yule? Lakini sioni sababu hasa, kama siri ya Maria, ndiko kusema wakati wa kutoka kwenda kupiga simu, mama yake na Agnesi wangalimwona na kunieleza.

Loo! Kisha sauti ile nikikumbuka vyema, naona ilikuwa ya mwanamume. Lo! Hivi sasa nakumbuka hata jina lake, nililiandika mahali ............ ndiyo hapa........ penye daftari langu. Eee! ni "Fambo" hakuna jina la pili, ila fambo tu. Basi nitakwenda kuwauliza kama wanamfahamu."

**41.** Ni nini ambacho Wingo alifikiria angalikuwa "nacho" endapo kisingalichukuliwa na mtu?
- A. Kiko chake
- B. Sigara ya sumu
- C. Simu
- D. Fambo

**42.** Msemaji anawashuku kina nani kuhusu kuiandaa sigara ya sumu?
- A. Agnesi na Maria
- B. Rafaili na Maria
- C. Maria na Yakobo
- D. Rafaili na Agnesi

**43.** Sigara hiyo ya sumu iliandaliwa kwa nia na lengo la:-
- A. kutia kwenye kiko
- B. Maria kuolewa
- C. Kupata sumu
- D. Kumwulia mzee Yakobo

**44.** Msimulizi anasema kuwa ni nani aliyepiga simu?
- A. Yakobo
- B. Maria
- C. Fambo
- D. Rafaili

**45.** Kulingana na kauli ya msimulizi, mle ndani mlikuwa na wanawake tu. Anamaanisha ndani wapi?
- A. Katika nduka la kuuzia sigara
- B. Alimofariki Mzee Yakobo
- C. Alimojificha Maria
- D. Alimopigia simu mtu

**46.** Msimulizi anasema ________
- A. Mzee Yakobo aliwasha kiko akavuta
- B. Wanawake walifanya njama ya kumwua Yakobo
- C. Maria aliondoka kwenda kupiga simu
- D. Katika habari hii kuna Agnesi, Maria na Mama Maria

**47.** Kwa nini msimulizi alisema, "Loo"?
- A. Alishtuka kwa furaha
- B. Alikumbuka alivyoambiwa
- C. Alikuwa na hofu
- D. Alikuwa ameshtuka kwa kukumbuka

**48.** Kulingana na taarifa, msemaji alitumia, "Eee!..........." kwa sababu ya:-
- A. kulikumbuka jina la mtu aliyepiga simu
- B. kumwita mwezake kwa furaha
- C. kumpongeza mwenzake
- D. kutuonyesha amefurahi kukutana na Fambo

**49.** Bila shaka "daftari" alilolitumia msemaji ni la kuandikia mambo au matukio ya kila siku. Je kwa Kiswahili mufti, daftari hilo la kunakilia matukio ya kila siku huitwaje?
- A. Tarakilishi
- B. Rununu
- C. Shajara au kitini
- D. Matini au makala

**50.** Jina la msimulizi wa habari hii ni ________
- A. Yakobo
- B. Fambo
- C. Bila shaka
- D. Wingo